**OR TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI NAMABENGO**

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE ( JOINING INSRUCTIONS)**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0744013033/ 0754096455**

**Makamu Mkuu wa shule 0768313628**

**Patron 0748414129**

**Shule ya Sekondari NAMABENGO**

**S.L.P 55**

**NAMTUMBO.**

**Tarehe 30/04/2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NAMABENGO HALMASHAURI YA NAMTUMBO MKOA RUVUMA MWAKA 2026**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2026 na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari NAMABENGO ipo umbali wa Kilometa 30 Mashariki mwa Mji wa Songea, Usafiri wa basi kutoka mjini Songea unapatikana katika kituo cha mabasi cha Majengo, panda daladala zilizoandikwa *NAMABENGO* Nauli ni Shilingi 2000.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ........... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe .............. Mwisho wa kuripoti ni tarehe………………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1. Sare za Shule**

a). Sare ya shule hii ni sketi 2 kijani jeshi yenye malinda kumi (10) na iachie sentimeta 15 kutoka ardhini.Wavulana suruali 02 rangi ya khaki yenye marinda mawili (siyo ngwasuma na siyo modo).Upana wa chini uwe kuanzia sentimeta 16 na kuendelea. ( ukaguzi utafanyika).

b). Mashati mawili meupe, mikono mifupi, kwa wavulana na wasichana. Kwa wanaotumia hijab (kijuba) ifanane na shati la shule na ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

c). Sare za michezo kwa shule hii ni trakisuti nyeusi kwa wasichana na wavulana zenye fito tatu nyeupe ubavuni, Pia kwa wanaokuja kusomea HGK na HGFa,Wawe na jezi ya taifa stars rangi nyeusi na HGL na HGLi Wawe na jezi ya taifa stars rangi ya bluu.Viatu vya michezo vyenye njumu na raba vyeupe kwa wote kwa matumizi ya mchaka mchaka.

d). Viatu vya shule, rangi vyeusi vinavyofungwa kamba vyenye visigino vifupi.

e). Soksi jozi mbili, nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.

f). Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana.

g). Sweta la rangi ya kijani jeshi shingo ya V.

h). Nguo za kushindia, (shamba dress) sketi damu ya mzee (wasichana) suruali damu ya mzee (wavulana) zenye vipimo kama vile vilivyoainishwa kipengele (a) hapo juu.

I). Fulana ya njano aina ya (form six) na hijab ya njano kwa wanafunzi wa kiislam (uje nayo).

J. T.shirt ya michezo aina ya taifa stars. Kwa watakao soma HGL NA HGLi wanunue tshirt taifa stars rangi ya blue . kwa watakao soma HGK na HGFa wanunue t shirt ya taifa stars rangi nyeusi.

NB; PICHA ZA SARE ZIMEAMBATANISHWA UKURASA WA MWISHO.

**2.2. Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo**

**shuleni:-**

i. Madaftari yasiyopungua 7.
ii. Ream 2(A4) ya karatasi (kwa mwaka).
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatishwa ).
iv. Godoro futi 2.5
v. Mashuka jozi 2 rangi ya bluu, blanketi 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya bluu.
vi. Nguo za ndani za kutosha.
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
viii. Ndoo moja kubwa ya lita 20 yenye mfuniko kwa matumizi ya shule, ndoo ndogo lita 10 yenye mfuniko kwa matumizi yake na galoni moja ya lita tano kwa matumizi ya maji ya kuywa mwanafu mwenyewe.
ix. (a) kwa watakao soma HGL waje na jembe moja lenye mpini na hard broom moja.
(b) kwa watakao soma HGLi waje na jembe moja lenye mpini na mooper moja.
(c) kwa watakao soma HGK waje na jembe lenye mpini na kwanza moja.
(d) kwa watakao soma HGFa waje na jembe lenye mpini na softbroom moja.
x. Awe na **BIMA YA AFYA.**

**3.0.Michango mbalimbali**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= |
| 3. | Nembo | 5,000/= |
| 4. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango iwekwe akaunti na 023101001161 NBC Jina NAMABENGO SEC. SCHOOL**

## 4.0. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 4.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**4.2. Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**5.0. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi

   wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Kivuli cha taarifa ya matokeo ya kidato cha nne. (result slip) na picha nne passport size
vi. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza

kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule.** ***Mwanzalila, Gabriel Simon***

**Mhuri wa Mkuu wa Shule**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0754096455**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0768313628**
- **Mwandamizi Taaluma 0762812445**
- **Mwandamizi Malezi 0748414129**

**<u>TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI.</u>**

Shule inapenda kupata taarifa muhimu za kila mwanafunzi kwa ajili ya mawasiliano Wakati wote awapo shuleni.

**<u>Fomu hii ijazwe kwa usahihi na ukamilifu</u>**.

Jina la Mwanafunzi………………………………………………………. Me/ke Kidato……………..tahasusi …………………..mwaka…………………… Anwani…………………………………. ya nyumbani (inayotumika).

Namba ya simu (ya Nyumbani/ya mzazi)……………………………………………………………….

Mtaa/Kijiji anachotoka……………………………Kata…………………………..

Tarafa……………………..

Wilaya…………………………..

Mkoa……………………………………………………………………………….

Shule ya Sekondari atokayo………………………………………………………………………………

Anwani ya Shule………………………………. Namba ya Mtihani ya Kidato cha Nne…………

Dini yake ni ……………………………………………….. (Mkristo, Mwislamu n.k.)

Sahihi………………………………………….

Tarehe……………………………………………………

**TAARIFA YA MZAZI/MLEZI.**

Jina la Mzazi/Mlezi………………………………………………………………………………
Anwani yake…………………………………………………………………………………
Namba ya simu………………………………………………………………………………
Kazi anayofanya………………………………………………………………………………
Wilaya/Mji anakofanyia kazi……………………………………………………………………
Anwani ya kazini……………………………………………………………………………
Namba ya simu ya kazini………………………………………………………………

**WATU WA KARIBU NA FAMILIA AMBAO UNGEPENDA WAPATE TAARIFA ZAKO ZAIDI YA WAZAZI/WALEZI.**

1.Jina…………………………………………………..
Anwani……………………………………………
Namba ya Simu……………………………… kazi anayofanya………………………………
Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………………………………
2.Jina……………………………………………
Anwani……………………………………………
Namba ya Simu……………………………… Kazi anayofanya
Uhusiano wake na mwanafunzi……………………………………………………………..
3.Jina………………………………………..
Anwani……………………………………………………..
Namba ya Simu………………………………… Kazi anayofanya…………………………..
Uhusiano wake na Mwanafunzi………………………………………………………

**AHADI.**

**A: MWANAFUNZI.**

Jina la Mwanafunzi……………………………………………………………………………
Anuani……………………………………………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………………………………………………
Mimi………………………………………………………………………………………………
Nimesoma maagizo ya Shule kwa makini na kuyaelewa, Naahidi kuwa mtiifu
Nitazingatia sheria. Taratibu za shule kama nitakavyoelekezwa.

**B: MZAZI/MLEZI.**

Mimi…………………………………………………… Mzazi/Mlezi wa ……………………
Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa yanayomuhusu mtoto

Wangu. Ninakubali kuwa mwanangu achukue nafasi hiyo. Ninaahidi pia nitashirikiana na Uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu
Kielimu na kitabia.
Sahihi ya Mzazi/Mlezi……………………………………….. Tarehe……………………

PMO- RALG
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

The Headmaster,

Namabengo Secondary School,
P.O.BOX 55.
Namtumbo.

**Part. A.**
**To Medical Officer**
……………………………………………………

Ref………………………………………………………………………………………………
…………………………………………….
(Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time Schooling course.

I. (a) Eye-Sight
(b) Hearing
(c) Limbs
(d) Speech
(e) Venereal Diseases
(f) Leprosy
(g) Epilepsy

II. Neuroses

III. Other serious diseases

**Part B. MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be Completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student and I consider that he/she is physically fit/unfit, mentally fit/unfit for a full time schooling course.

a. Eye-sight………………………………….
b. Hearing…………………………………
c. Limbs………………………………………
d. Speech………………………………………

II. Neuroses……………………………………………………………………………………..

(III) Other Serious diseases …………………………………………………………………….

Date…………………………………………Signature…………………………………………

Station…………………………………… Designation…………………………………….